MKOA WA KABARE WAKAA JUU YA MAKAA YA MOTO

Bwito yatikisika

Hapo majuzi, siku ya kwanza tarehe 27 may 1985, mwananchi Karhebwa Kanyabalirwa, makamu wa prezidenti wa Baraza la washauri katika mkoa wa Kabare, alifariki dunia baada ya kupigwa panga mara mbili na warugaruga wawili. Kitendo hicho cha uovu kilifanyika kunako mlima wa Maya ambao hupatikana kati ya mitaa ya Kabare na Bagira wakati mwananchi Karhebwa alikuwa akirejea nyumbani mtaani Bagira toka kazini huko Kabare.

Yasemekana kuwa kifo cha mwananchi Karhebwa kimeamsha chuki na uwoga mkali kati ya wakaaji wa Kabare na Bagira. Kufuatana na habari hiyo, watu kazaa walikuwa wakinongonezana "Tumemlaza" na wengine kusema "Damu itamwangika", ebu, labda si uwongo kufuatana na hali iliyoko kwa sasa.

Kulingana na uchunguzi unaofanyika, majina ya wananchi 8 yapo daftarini. Ni kati yao kwazaniwa wauaji wa mwananchi Karhebwa. Mmoja wao ni Kabungwe (Protaz) anayejulikana kuwa muuaji wa tangu zamani. Watu hujiuliza sasa ni nani aliyewatuma ? Hapa hakuna jibu kamili, kwani labda wengine hujilipisha kisasi. Daftari ya majina mengine yapo tayari. Na kati ya watu wanaopashwa kuwawa na waliokwisha kuwawa ni wananchi Lugamba, Vuningoma, Karhebwa, (waliopata kifo), Chiribagula, Kasaza, Chigangu na Mongane (mbunge wa zamani)

Kifo cha mwananchi Karhebwa kimechemsha mambo yote ya zamani na kutia wasiwasi mkoani. Ingawa siku si nyingi, Prezidenti wa chama na Liwali wa jimbo, mwananchi Mwando Nsimba aliwasili mkoani Kabare. Huko aliwatolea wakaaji mashauri muhimu kwa kulinda amani kwa maendeleo bora wa mkoa wao.

Kwa nini Karhebwa kawawa ?

Kuwawa kwa mwananchi Karhebwa kwatokana, wasemavyo, na kiasi cha zaire 1.350.000 alizopewa kwa kutoa rushwa (kuhonga, corrompre) kwa viongozi kazaa wa wizara ya uongozi wa nchi ili nchi ya Bushi igawanyike.

Ufuatano ukarasa 10

UAKILI WA UCHUNGUZI WA MISHAHARA WAFEZEESHWA

Ebu! Mambo yamegeuka kunako uakili(commission) wa uchunguzi wa mishahara. Ingawa hao wanaohusika na hesabu na malipo ya mishahara (comptables) walivunduliwa na kupelekwa mbele ya waamzi na kuachishwa kazi, wamerudishwa kazini kwa mshangao mkubwa.

Wamoja kati yao wamekwisha tena aanza kazi na wengine hujitayarisha kurudi kazini bila vikartasi halali vinavyowaruhusu wakati wa uchunguzi muhimu uliofanyika uligundua magendo yao na pesa nyingi kurudishwa katika sanduku la serkali.

Mnamo mwezi wa pili, serkali imerudishwa kiasi cha zaïre1.588.000 Kiasi hicho cha feza kilijulishwa mnamo tarehe 13 Aprili 1985.

Kufuatana na masemi ya prezidenti wa uakili huo, mwananchi Endjonga, makamu wa liwali wa jimbo, feza hizo ziliwekwa kwenyi kituo cha Benki kuu la Zaïre mjini Bukavu baada ya uchunguzi uliofanyika na uakili (commission) uliotumwa na Baraza la waziri.

Kulingana na mwendo wa kazi uliochukuliwa na wanamemba wa uakili huo toka Kinshasa, mwenendo huo haukufurahisha wakuu wa jimbo. Kwa hiyo wakuu hao walishtaki wanamemba hao kwenyi korti ili waamzi wachungue kwa karibu swali hilo. Kwani wao pahali ya kufanya uchunguzi walijiruhusu kujitia nafasi ya walipaji wa feza na mishahara (comptables) na hata kutia sahihi kunako vikartasi vya feza ingawa hawaruhusiwe.

Lakini kitu kinachoshangaza ni kuona mashtaki hayo yalitupiliwa mbali kutokana na hatua zilizochukuliwa na wakuu mjini Kinshasa. Na kufuatana na hatua hiyo, walipaji wa feza na mishahara walirudishwa kazini ingawa pia uwerevu wao wa kupokonya mishahara ya wafanyakazi waliofariki dunia, kuacha kazi ao kupumzishwa uligunduliwa.

Basi, mahitaji ya watu wote ni kuona uakili wa jimbo kuendelea na kazi zake za uchunguzi. Kwani kisha uchunguzi wa mwezi wa pili na wa tatu, tutapigwa na bumbuazi wakati wa malipo ya mishahara miezi ijayo kutokana na upungufu ao upokonyaji wa feza na mishahara ya wafanyakazi.

Bisimwa L.B. Tserou.

JUA

Gazeti la Kivu

Mwaka wa 12 no 278 — Tarehe 15 mpaka 21 juni 1985

Kiongozi : Mutiri - wa - Bashara.

Kamati kuu ya chama

Mareshali MOBUTU kakusanya wanamemba wa chumba imara.

Habari toka Kinshasa zajulisha kuwa, Mareshali wa Zaïre, Mobutu Sese Seko, Prezidenti-muundaji wa Chama cha Mapinduzi, aliwakusanya wanamemba wa Chumba imara cha Kamati kuu ya Chama na wakuu mbalimbali nchini kunako makao yake ya Kampi Koloneli Tshatshi. Mkutano huo wa Kinshasa ni mwendeleo wa uliofanyika tarehe 2 juni 1985 mjini Gbadolite, katika jimbo la Ekwatori.

Ukomo wa mkusanyo huo ulikuwa wa kuchungua kwa karibu hali ya mwelezo wa siasa na kijamii nchini. Pia namna gani kutayarisha sherehe za kumbokumbo ya miaka 25 tangu pale nchi Zaïre ilijinyakulia uhuru wake mnamo tarehe 30 Juni 1960. Tatizo la tatu lilikuwa lile la wale wakafri wa 7 waliotaka kutia vitisho na mchafuko nchini toka Lybia ya mharamia Kadhafi ambako walifunzwa. Tena wakuu hao walichungua kwa karibu matangazo ya mwananchi Nguz a Karl-i-Bond, waziri mkuu wa zamani wa Zaïre ambaye aomba kurejea nchini baada ya kujiuzulu nchini Ubeleji. Na kwa hiyo inajulishwa kama milango ipo wazi kwa mwananchi wowote atakaehitaji kurejea makwao kwani kwa mtu ni kwa mtu na mgeni haoni mbaramwezi.

Kulingana na tarehe hiyo ya 12 Juni, tutawakumbusha kama ni tarehe hiyo Baba wa Taifa, Marechali Mobutu kapambana pamoja na askari-jeshi halali katika vita vya Kamanyola na kuwasaga vikali wahuni "Mulele mai". Kufuatana na siku hiyo maonyesho ya vitu, vitabu mbalimbali yalifanyika juu ya historia ya nchi Zaïre. Kahuzuria kwenyi maonyesho hayo, mwananchi Kasongo Mukundji, Prezidenti wa Bunge kuu la Taifa miongoni mwake mukiwa wakuu kazaa.

Je umesikia ...?

KAMA mbwa halali na mafuta tumboni ? Huyo bibi anayejidai kuwa mchuuzi, akijiruhusu kuuzisha risasi kimagendo baada ya "kujimwanga porini" mjini Bukavu toka Goma alishikwa mateka ?

Kwa kweli alipotaka kuingia katika ndege la VAC na kujielekeza Bukavu, akajionea cha mtema kuni kwani alizibiwa na katika sanduku lake, musishangae, mulikuwako risasi nyingi.

Kuona hivyo, akaanza kumtusi rubani na kumhamakia bila sababu juu ya haya kama mbweha mtegoni. Na bila kusahau, asemavyo mungwana, kama mkamatwa na ngozi ndiye mwizi.

KWAMBA mlevi wa mvinyo hulevika na mlevi wa mali halevuki? Kwa nini ? Hum, alaala ! Makamu wa mwenyekiti wa mataa wa Bagira mwananchi S... ajifezeesha. Kwani baada ya kutubu kosa zake na kurudishwa kazini kwa njia isiyo halali akisaidiwa na... ajiruhusu kumkania mzee "Gazeti JUA" eti atamsaga.

Mama Bobi Ladawa awasaidia wagonjwa

Mjini Kinshasa, mke wa Raïs wa Jamhuri, Mama Bobi Ladawa aliwatumia viongozi na wagonjwa wa Hospitali kuu Mama Yemo dawa na vifaa vingi kwa matibabu ili mwelezo wa kuimarisha mpango wa miaka saba ya kijamii utimizwe barabara.

Dawa na vifaa hivyo vilitolewa kwa jina ya Mama Bobi Ladawa na katibu wake wa pekee hospitali walimshukuru Mama Bobi Ladawa kwa moyo wake wa Kimama kwani vitu hivyo vilifika wakati ukosefu wavyo ulikuwa ukiwasonga.

Habari za Popote

Italia

Bwana Ali Agça aliyetaka kumuua Baba Mtakatifu wa Roma, Papa Yoane - Paolo wa pili alieleza mbele ya waamzi ya kuwa silaha aliyotumia kwa kumpiga Baba Mtakatifu risasi na hivi kumuondowa kunako ubalozi wa Urusi, mjini Sofia, mji mkuu wa Bulgaria. Waumini na watu wengi ulimwenguni hujiuliza kisa gani kilichowatuma Warusi kutaka wamuue Baba Mtakatifu wa Roma, Yoane-Paulo wa pili.

BISIMWA L.B.